SHIRIKA LA RELI TANZANIA

Jarida la

# RELI NA MATUKIO

Toleo namba 27, Machi 2023

Habari | Makala | Matukio | Elimu | Picha

# WAZIRI MKUU ASHUHUDIA RELI ILIYOTANDIKWA, MRADI WA SGR MWANZA – ISAKA WAFIKA 28%



Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa akizungumza na wananchi wa Nyashimbi mara baada ya kukagua reli iliyotandikwa alipotembelea mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa - SGR Mwanza - Isaka, mkoani SImiyu, Machi 2023

Na Mwandishi wetu

Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa ameshuhudia reli iliyoanza kutandikwa katika mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa – SGR Mwanza – Isaka akiwa katika ziara ya kikazi mkoani Simiyu, Machi 2023.

Mhe. Waziri Mkuu ametembelea mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa kuanzia eneo la Nyashimbi hadi Malampaka mkoani Simiyu kwa lengo la kukagua na kuona maendeleo ya mradi wa SGR Mwanza – Isaka uliofikia asilimia 28 huku kazi ya ujenzi wa Stesheni na utandikaji reli ikiwa inaendelea kwa kasi.

"Ziara yangu leo Maswa hapa Malampaka ni kuja kukagua reli ya kiwango cha kimataifa inayoendesha treni kwa kutumia umeme na hapa Malampaka kitajengwa kituo kikubwa cha abiria na mizigo aina

Inaendelea Uk. 2

## MIAKA MIWILI YA RAIS DKT. SAMIA, HAKUNA KILICHOSIMAMA Uk. 3 & 4



# WAZIRI MKUU ASHUHUDIA RELI ILIYOTANDIKWA, MRADI WA SGR MWANZA – ISAKA WAFIKA 28%

Inatoka Uk. 1

zote, hii reli nimeikagua mpaka naingia hapa inaendelea kujengwa viwango vyake ni vya kimataifa na itatumia muda mchache abiria na mizigio kufika hapa" alisema Waziri Mkuu

Waziri Mkuu amewataka wananchi wa kata ya Malampaka kuchangamkia fursa zilizopo katika mradi wa reli ya kisasa pamoja na kituo cha abiria na mizigo kitakachojengwa ili kuwaongezea kipato na kukuza uchumi.

"Niko mkoani Simiyu kwa siku tatu kukagua miradi ya maendeleo inayojengwa nimeona miradi yenu mingi imefikia hatua nzuri, mingine imekamilika imeanza kufanya kazi, nimekuja kuona reli kazi zinaendelea. Reli hii itaweka kituo hapa Malampaka jipangeni hususani katika upimaji ardhi na kutoa hati, hii reli inajengwa kwaajili yenu" alisema Waziri Mkuu

Waziri Mkuu ameeleza kuwa ikiwa ni miaka miwili ya uongozi wa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan miradi inaendelea na imefikia hatua nzuri. Malengo ni kukamilisha utekelezaji wa ilani ya CCM angalau kwa asilimia 95 ifikapo mwaka 2025.



Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa akipata utambulisho wa menejimenti na baadhi ya watumishi wa TRC alipowasili kijiji cha Nyashimbi kukagua maendeleo ya mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa - SGR Mwanza - Isaka mkoani Simiyu, Machi 2023

Wananchi wa Malampaka waliohudhuria mkutano wa Waziri Mkuu wamesema kuwa wamefurahishwa na ujio wa mradi wa SGR na wanaamini kuwa utaleta manufaa kiuchumi hivyo wamejipanga kuchangamkia fursa zitokanazo na mradi ikiwemo kujenga nyumba za wageni, viwanda vya kuchambua pamba na kuboresha kilimo kwa kutumia umwagiliaji kwani kutakuwa na uhakika wa usafiri wa mazao kwenda kwenye masoko ya ndani na nje.



Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa akipata maelezo kutoka kwa Mkurugenzi Mkuu TRC Masanja Kadogosa kuhusu mpangilio na maeneo inayopita reli ya kisasa - SGR kipande cha Mwanza - Isaka alipofanya ziara kukagua mradi mkaoni Simiyu, Machi 2023

# MIAKA MIWILI YA RAIS DKT. SAMIA, HAKUNA KILICHOSIMAMA

**Na Mwandishi wetu**

Samia Suluhu Hassan ni Rais wa sita wa Tanzania ambaye pia ameweka rekodi ya kuwa mwanamke wa kwanza kushika wadhifa huo wa juu zaidi nchini Tanzania, Rais Dkt. Samia ameingia madarakani mnamo mwezi Machi 2021 baada ya kifo cha mtangulizi wake hayati Dkt. John Pombe Magufuli ambapo awali Rais Samia alikua Makamu wa Rais tangu mwaka 2015.

Rais Samia Suluhu Hassan amekuwa akiendeleza miradi mbalimbali ya kimkakati tangu alipoachiwa kijiti cha uongozi wa kuwa Rais wa nchi pamoja na kufungua miradi mipya ambayo yote kwa pamoja itakwenda kuongeza kasi ya ukuaji uchumi wa taifa la Tanzania, moja ya miradi hiyo mikubwa ya kimkakati ni pamoja na Mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa – SGR unaosimamiwa na Shirika la Reli Tanzania.

Mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa katika awamu ya kwanza umegawanyika katika vipande vitano ambavyo kipande cha kwanza kutoka Dar es Salaam hadi Morogoro chenye urefu wa kilomita 300, kipande cha pili kutoka Morogoro hadi Makutupora chenye urefu wa kilomita 422, kipande cha tatu Makutupora hadi Tabora chenye urefu wa kilomita 368, kipande cha nne Tabora hadi Isaka chenye urefu wa kilomita 165, na kipande cha tano Isaka hadi Mwanza chenye urefu wa kilomita 341.




Muonekano wa jengo la stesheni ya reli ya kisasa - SGR Kilosa mkoani likiwa limekamilika.



Muonekano wa jengo la ofisi ya makao makuu ya Shirika la Reli Tanzania lililojengwa chini ya mkataba wa ujenzi wa reli ya kisasa - SGR kipande cha Morogoro - Makutupora katika kipindi cha miaka miwili ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, eneo la Kikuyu jijini Dodoma.

Inaendelea Uk. 04



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akishuhudia utiaji saini wa mkataba wa ujenzi wa reli ya kisasa - SGR awamu ya pili, kipande cha kwanza Tabora - Kigoma (KM506) kati ya Shirika la Reli Tanzania - TRC (kushoto) na wakandarasi kampuni ya CCECC, Ikulu jijini Dar es Salaam, Disemba 2022.

# MIAKA MIWILI YA RAIS DKT. SAMIA, HAKUNA KILICHOSIMAMA

Inatoka Uk. 03

Wakati Rais Samia Suluhu Hassan ameingia madarakani Mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa ulikua na urefu wa takribani kilomita 722 ambapo ameanzisha ujenzi mpya wenye urefu wa takribani kilomita 1200 wa reli hiyo ya kisasa ambapo kwa ujumla wake hadi sasa ni kilomita 1921 kwa vipande vyote. Ahadi ya fedha za uendeshaji wa mradi huo wakati anaingia ilikua ni Trilioni 7.3 shilingi za kitanzania na hadi sasa zimeongezeka hadi kufikia Trilioni 23.3 shilingi za kitanzania.

Hata hivyo Rais Samia Suluhu Hassan katika kipindi cha miaka miwili amefanikiwa kuanzisha miradi ya ujenzi wa reli ya kisasa katika kipande cha tatu cha Makutupora – Tabora chenye thamani ya dola Bilioni 1.9 za kimarekani zenye thamani ya shilingi Trilioni 4.4 za kitanzania, pia kipande kingine alichokianzisha ni kipande cha nne Tabora – Isaka chenye thamani ya dola za kimarekani milioni 600.1 sawa na shilingi Trilioni 2 za kitanzania, vilevile Mhe. Rais alizindua kipande cha tano Isaka – Mwanza wenye thamani ya dola Bilioni 1.326 za kimarekani sawa na shilingi Trilioni 3.06 za kitanzania na pia TRC imesaini mkataba wa kipande kingine cha ujenzi wa reli ya kisasa kutoka Tabora – Kigoma chenye urefu wa kilomita 506 chenye thamani ya shilingi Trilioni 6 fedha za kitanzania.

"Uwekezaji pamoja na uendelezaji wa miradi aliofanya Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan tunautafsiri kwenye reli kwa namna mbili zifuatazo, ya kwanza



Muonekano wa ndani wa mabehewa ya reli ya kisasa - SGR yaliyowasili nchini katikia kipindi cha miaka miwili ya Rais D.kt Samia Suluhu Hassan.



Muonekano wa kicha cha treni za umeme kwaajili ya reli ya kisasa

ni kumalizia miradi ambayo iliyokuwa ikitekelezwa katika awamu ya tano ikiwemo ujenzi wa vipande viwili amavyo vilikuwa kwenye uwiano kwa kipande cha kwanza Dar es Salaam – Morogoro kilikua na asilimia 70 na kipande cha pili Morogoro – Makutupora kilikuwa na asilimia 60 ambapo kwa sasa Kipande cha kwanza Dar es Salaam – Morogoro umefikia asilimia 97.9 na kipande cha pili Morogoro – Makutupora umefikia asilimia 92.8 na tafsiri ya pili wakati anaingia Mhe. Rais miradi ilikuwa na kiasi cha shilingi Trilioni 7.8 ambapo miradi hiyo imeendelea kutekelezwa" amesema Mhandisi Machibya Masanja.

Pia ujenzi wa reli ya kisasa unaenda sambamba na ununuzi wa vichwa pamoja na mabehewa ambayo yatafanya kazi punde uendeshaji wa reli hiyo utakapoanza, hadi sasa Serikali ya Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan imepokea mabehewa 14 kati ya 59 yaliyotengenezwa na kampuni ya Sun Shin Rolling Stock Technology (SSRST) iliyopo nchini Korea ya Kusini na pia Serikali ya Tanzania imetoa takribani Dola za Kimarekani milioni 295.74 kwa kampuni ya Hyundai Rotem ya Korea ya Kusini kwaajili ya ununuzi wa vichwa vya treni vya umeme 17 na seti za treni za kisasa (Electric Multiple Unit – EMU) 10 na 'Locomotive simulator' 1 ya umeme, pia kuna mabehewa 1,430 ya mizigo ambayo yapo katika matengenezo.

Ni dhahiri kwamba Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan amechukua hatua madhubuti zinazolenga kuimarisha uchumi wa Tanzania katika sekta ya usafirishaji wa reli kwa kukuza miundombinu ya reli nchini pamoja na kuweka mazingira wezeshi ambayo hayakwamishi mradi wa ujenzi reli ya kisasa  kwa vipande vyote vitano ambavyo ujenzi wake unaendelea na vingine vikiwa mbioni kukamilika.

# KAMATI YA BUNGE YA MIUNDOMBINU YARIDHISHWA NA MAENDELEO YA MRADI WA SGR, WIZARA, TRC WAPONGEZWA



Kaimu Mkurugenzi wa Mawasiliano, Ishara na Umeme TRC Mhandisi Mateshi Titto (kulia) akiwaelezea wajumbe wa kamati ya Bunge ya Miundombinu kuhusu mifumo ya mawasiliano itakayojengwa katika jengo la Stesheni ya reli ya kisasa jijini Dodoma, Machi 2023.

**Na Mwandishi wetu**

Kamati ya Bunge ya kudumu ya Miundombinu yaridhishwa na maendeleao ya mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa – SGR baada ya kukamilisha ziara kukagua mradi kutoka Dodoma hadi Dar es Salaam iliyofanyika kwa siku mbili kuanzia Machi 14 hadi 15, 2023.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu Mhe. Selemani Kakoso ameridhishwa na maendelea ya mradi kipande cha Morogoro – Makutupora ambacho kimefikia zaidi ya asilimia 82 na kipande cha Dar es Salaam - Morogoro ambacho kimefikia zaidi ya asilimia 9, kazi kubwa iliyobaki ni ujenzi wa reli kuelekea bandarini jijini Dar es Salaam.

"Nimeridhishwa na maendeleo ya mradi, naipongeza Wizara na TRC kwa kazi kubwa mliyofanya, nawaahidi mtakapoleta maombi yenu ili yaweze kuidhinishwa kupitia Wizara yako Mhe. Waziri sina shaka pamoja na Wabunge walioona kazi hii tutayapitisha bila kumkwamisha Mhe. Rais" alisema Mhe. Kakoso

Mhe. Kakoso alisisitiza kuwa "Tumefanya ukaguzi kutoka Dodoma hadi Morogoro na hatimaye tumefika Dar es Salaam, naipongeza Serikali kwa kazi ambayo imefanya kujenga miundombinu ya reli ya kisasa, dhamira ya Serikali tumeiona na tumejiridhisha"

Kamati pia imefanya ziara katika Karakana ya Vichwa vya treni mkoani Morogoro kwa lengo la kukagua utendaji wa karakana hiyo pamoja na kuona namna ya kuishauri Serikali jinsi ya kuboresha ufanisi wa kazi katika karakana ili kuleta tija katika huduma ya usafirishaji kwa njia ya reli na kukuza uchumi.

"Tumekagua karakana ya reli inayokarabati na kutengeneza vichwa vya treni mkoani Morogoro, na leo tumekagua reli kwakweli miundombinu inajengwa niwahakikishie wananchi kuwa ujenzi umefikia hatua nzuri sana" alisema Kakoso

**Inaendelea Uk. 6**

# KAMATI YA BUNGE YA MIUNDOMBINU YARIDHISHWA NA MAENDELEO YA MRADI WA SGR, WIZARA, TRC WAPONGEZWA

Inatoka Uk. 5

Naibu Waziri wa Uchukuzi Mhe. Atupele Mwakibete ameishukuru kamati na kusema kuwa kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi ameyapokea maelekezo na ushauri ikiwemo suala la mabehewa na vichwa vya treni ambalo linaendelea kufanyiwa kazi ambapo hadi kufikia mwezi Aprili 2023 vichwa vya treni vinatarajiwa kuwasili ili kuanza kutoa huduma ya usafiri Dar es Salaam – Morogoro.

"Nichukue fursa hii kwa kuishukuru kamati ya bunge ya miundombinu kwa kulitembelea Shirika la reli, pia kwa maoni yao na mara kadhaa wamekuwa wakitoa maoni na Serikali imekuwa ikiyafanyia kazi, nawapongeza watumishi wote na Mwenyekiti wa Bodi pamoja na Mkurugenzi Mkuu wa TRC kwa usimamizi mzuri" alisema Mhe. Mwakibete

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi TRC Prof. John Kondoro amesema kuwa amefarijika na maelezo na maelekezo ya kamati kwani inaashiria kuwa wameridhika na maendeleo ya mradi, pia maelekezo ambayo yametolewa na kamati Uongozi wa Shirika umeyapokea kwaajili ya kuyatekeleza.

Kamati imetoa ushauri kwa Serikali ikiwemo kuongeza kasi ya ukamilishaji wa mradi, kuajiri wafanyakazi ambao watakwenda kuendesha mradi, kusimamia ununuzi wa vitendea kazi ikiwemo mitambo, mabehewa na vichwa vya treni pia kamati imeitaka Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi ishirikiane na Wizara ya Nishati ili kuwepo na nishati ya uhakika itakayowezesha shughuli za uendeshaji wa reli ya kisasa.



Meneja Msaidizi wa mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa - SGR Dar es Salaam - Morogoro Mhandisi David Msusa akiwaelezea wajumbe wa kamati ya bunge ya miundombinu kuhusu chumba cha kuongozea treni kilichopo ndani ya jengo la Stesheni ya SGR jijini Dar es Salaam, Machi 2023.



Fundi katika karakana ya vichwa vya treni Morogoro Bwana James Mlosa akiwaelezea wajumbe wa kamati ya bunge ya miundombinu kuhusu ukarabati wa bogi (inayoonekana pichani) ya kichwa cha treni walipotembelea Karakana mkoani Morogoro, Machi 2023.



Meneja Karakana Mhandisi Kelvin Kimario akiwaelezea wajumbe wa kamati ya bunge ya miundombinu kuhusu ukarabati wa magurudumu ya treni walipofanya ziara katika Karakana ya vichwa vya treni mkoani Morogoro, Machi 2023.



Mwenyekiti na Wajumbe wa kamati ya Bunge ya Miundombinu wakiwa katika picha na Naibu Waziri wa Uchukuzi, Menejimenti na Wafanyakazi wa TRC walipotembelea handaki namba 2 Kilosa mkoani Morogoro, Machi 2023.

# WANAWAKE CCM WATEMBELEA MRADI WA SGR, WAMPA HEKO RAIS SAMIA

**Na Mwandishi Wetu**

Baraza la Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT) kutoka Chama cha Mapinduzi (CCM) wamefanya ziara katika mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa kutoka Dar es Salaam hadi Dodoma na kumpongeza Rais Samia kwa uthubutu wa kuendeleza mradi wa SGR katika kipindi cha miaka miwili ya uongozi, Machi 2023.

Wajumbe wa Baraza wamefanya ziara kwa kutumia treni ya uhandisi ya mkandarasi kwa lengo la kuona maendelea ya mradi na kusherekea mafanikio ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan katika miaka miwili ya uongozi wake.

Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake Tanzania Bi. Mary Chatanda amesema “tumejionea wenyewe kwa kupita kila kituo mambo ni mazuri hatuna budi kumpongeza Mhe. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea na miradi ya kimkakati, hakika Mwanamke mwenzetu ameweza ndio maana jana sisi wanawake wa UWT Taifa tumeamua kumpongeza kwasababu ametuheshimisha.”

Aidha, kabla ya ziara Baraza la Umoja Wanawake Tanzania liliandaa kongamano la kusherekea na kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano Tanzania Mhe. Dkt Samia Hassan Suluhu kwa kutimiza miaka miwili ya uongozi katika uwanja wa Uhuru, jijini Dar es Salaam ambapo Wanawake kutoka Shirika la Reli Tanzania walishiriki.

Katika Kongamano hilo Rais Samia alisema kuwa hakuna mradi uliosimama kutekelezwa tangu amechukua madaraka ya Urais Machi 2021 katika nyanja zote ikiwemo sekta ya Maji, Usafirishaji na Elimu vyote vinaendelea vizuri.

Katibu Mkuu wa UWT Taifa Dk. Philis Nyimbi amesema katika kusherekea miaka ya miwili ya Rais Samia Suluhu Hassan Tanzania imeshuhudia ujenzi wa reli ya kisasa (SGR) ukiendelea katika vipande vinne ambavyo ni Morogoro - Makutupora, Makutupora - Tabora, Tabora - Isaka pamoja na Isaka - Mwanza.

"Tunaona miundombinu ya reli, barabara imeimarika na ujenzi wa madaraja yenye viwango kuanzia vijijini hadi mijini." ameongeza Dk. Philis.




Meneja Msaidizi wa Mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa - SGR Morogoro - Makutupora Mhandisi Oliver Kilyenyi (wa pili kushoto) akiwaelezea wajumbe wa baraza kuu la wanawake Tanzania kuhusu ujenzi wa mahandaki Kilosa mkoani Morogoro, Machi 2023.



Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania - TRC Masanja Kadogosa (aliyevaa shati jeupe) akiwaonesha wajumbe wa Baraza kuu la Wanawake Tanzania sehemu yenye saini ya Hayati Dkt. John Pombe Magufuli ndani ya handaki refu la mradi wa SGR Kilosa mkoani Morogoro, Machi 2023

# KAMATI YA BUNGE PIC YAIPONGEZA SERIKALI KWA KUENDELEZA MRADI WA SGR

**Na Mwandishi wetu**

Kamati ya bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma ikiongozwa na Mwenyekiti wa kamati Mhe. Jerry Silaa yafanya ziara katika mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa – SGR Mwanza – Isaka, Machi 28, 2023.

Kamati imefanya ziara ikiwa na lengo la kuona maendeleo ya mradi pamoja na kuona thamani ya uwekezaji wa mitaji ya umma ambapo Serikali imewekeza fedha nyingi kutekeleza mradi wa SGR kuanzia Dar es Salaam kuelekea Kigoma na Mwanza.

"Sisi tumekuja kuangalia uwekezaji wa mitaji ya umma, Serikali inawekeza fedha nyingi, vipande hivi sita vina thamani ya takribani Dola za Marekani Bilioni 10 kwahiyo ni uwekezaji mkubwa ambao watanzania wanapaswa kujua lakini vilevile Bunge kusimamia na kuishauri Serikali" alisema Mhe. Silaa

Mhe. Silaa amesema kuwa mradi wa SGR ulianza muda mrefu lakini mpaka kufikia 2021 Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan alipoingia madarakani kulikuwa na vipande viwili ambavyo ni Dar es Salaam – Morogoro na Morogoro - Makutupora, lakini katika kipindi cha miaka miwili ya Dkt. Samia vipande vyote vina wakandarasi na kazi inaendelea.

"Kamati leo imefanya ziara kukagua TRC ambayo inasimamia mradi wa SGR inayojengwa kuanzia Dar es Salaam hadi Mwanza na Disemba 2022 Serikali ilisaini mkataba wa ujenzi wa reli ya kisasa kutoka Tabora hadi Kigoma" alisema Mhe. Silaa



Meneja mradi wa SGR Mwanza - Isaka Mhandisi Christopher Calist akimuelezea Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya umma Mhe. Jerry Silaa (wa pili kulia) kuhusu reli ya kisasa (haipo pichani) iliyotandikwa eneo la Nyashimba mkoani Simiyu, Machi 2023.

Mwenyekiti kwa niaba ya Kamati amepongeza na kuwatia moyo TRC wanaosimamia mradi na kusema kuwa kipande cha Mwanza - Isaka kimeshakamilishwa kwa asilimia 28 hadi kufikia Februari 2023, kazi inaenda vizuri, pia ameipongeza Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayoongozwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendeleza miradi yote ya kimkakati.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi TRC Prof. John Kondoro amesema kuwa "Tumepokea kamati ya bunge ya uwekezaji wa mitaji ya umma na wamekuja kutembelea mradi, kuna mambo ambayo wameona na wameeleza. Maendeleo ya mradi ni mazuri kwasababu mkandarasi yuko ndani ya mpango kazi uliowekwa katika hatua za kukamilisha mradi ambao mpaka sasa yuko asilimia 28, tunaamini kwa kasi anayokwenda nayo atamaliza ndani ya muda uliopangwa"

Mwenyekiti na Wajumbe wa Kamati ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma ambao ni wawakilishi wa wananchi walipata fursa ya kuona kazi iliyofanyika na wameangalia maendeleo ya mradi kwa ujumla, wameona vipande ambavyo tayari vimeshajengwa, wameona sehemu mbalimbali ambazo maandalizi tayari ikiwemo jijini Mwanza kwaajili ya ujenzi wa daraja, wametembelea Seke kuona kiwanda cha mataruma ambacho kinazalisha mataruma 1,600 kwa siku.

Katika hatua nyingine Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma imefanya ziara katika karakana ya vichwa vya treni na mabehewa na Chuo cha Reli Tabora (TIRTEC) Machi 2023 kwa lengo la kujionea uwekezaji mkubwa, kazi zinazofanywa na Shirika la Reli Tanzania - TRC na kuangalia namna kazi zinazofanywa zinakwenda sambamba na ujenzi wa reli ya kisasa – SGR ikiwa ni sehemu ya maandalizi ya uendeshaji wa mradi.

Menejimenti ya Shirika la Reli Tanzania imepokea maelekezo yaliyotolewa na kamati kuhakikisha Shirika linasimamia mradi uweze kuisha ndani ya muda uliopangwa kwani ni matarajio ya Serikali na Wananchi kwamba mradi utaisha kwa wakati ili waweze kunufaika na kile walichowekeza.

# MATUKIO KATIKA PICHA



Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa akizungumza na wananchi wa Nyashimba mara baada ya kukagua reli iliyotandikwa alipotembelea mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa - SGR Mwanza - Isaka, mkoani SImiyu, Machi 2023.



Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa akipata maelezo kutoka kwa Kaimu Mkurugenzi wa Ujenzi na Miundombinu ya Reli Mhandisi Machibya Masanja kuhusu viwango vya reli vinavyotumika katika mradi wa SGR Mwanza - Isaka, Machi 2023.



Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa akipata maelezo kutoka kwa Mkurugenzi Mkuu TRC Masanja Kadogosa kuhusu mpangilio na maeneo inayopita reli ya kisasa - SGR kipande cha Mwanza - Isaka alipofanya ziara kukagua mradi mkaoni Simiyu, Machi 2023.



Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa kamati ya bunge ya uwekezaji wa mitaji ya umma, Mwenyekiti wa Bodi TRC, Kaimu Mkurugenzi Mkuu TRC, Mkuu wa Chuo cha Reli Tabora na menejimenti ya TRC wakiwa katika picha mara baada ya ziara mkoani Tabora, Machi 2023.




Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi TRC Prof. John Kondoro akiwaelezea wajumbe wa kamati ya bunge ya uwekezaji wa mitaji ya umma kuhusu uwekezaji unaotarajiwa kufanyika katika Chuo cha Reli Tabora walipofanya ziara mkoani Tabora, Machi 2023.

# KIKAO KAZI CHA BARAZA LA WAFANYAKAZI TRC, WAJUMBE WATEMBELEA MRADI



Katika picha ya pamoja ni wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi TRC walipotembelea mradi wa SGR kipande cha kwanza Dar es Salaam - Morogoro katika stesheni ya SGR mkoani Morogoro hivi karibuni, 2023.

**Na Mwandishi wetu**

Shirika la Reli Tanzania - TRC limefanya kikao cha baraza la wafanyakazi TRC jijini Dar es Salaam katika ukumbi wa Bandari tarehe 30 na 31 mwezi Machi 2023.

Kaimu Mwenyekiti wa Baraza la wafanyakazi TRC Vincent Tangoh amesema lengo la kikao cha baraza la wafanyakazi ni kumshauri mwajiri kwa kushirikiana na menejimenti namna ya kuendeleza Shirika, baraza limeundwa na wawakilishi wa wafanyakazi kutoka idara na kanda zote.

"Baraza hili limeundwa kwa mujibu wa Sheria na hii inasaidia kwa wafanyakazi kupata ushirikishwaji wa majukumu yote yanayoendelea ndani ya shirika" amesema Tangoh.

Mwenyekiti wa Chama cha Wafanyakazi wa Reli (TRAWU) Bwana Godfrey Siwingwa amesema baraza litasaidia kutatua changamoto zinazowakabili wafanyakazi katika idara na Kanda zote kupitia wawakilishi kwa kushirikiana na menejimenti.

"Kwahiyo hili baraza litasaidia sana wafanyakazi kujua na kupata haki zao stahiki kutoka kwa mwajiri, pia menejimenti itapata haki ya kuwaambia wajumbe nini kifanyike kwa wafanyakazi ili kuweza kutimiza malengo ya kuboresha shirika" ameongeza Godfrey Siwingwa.

Aidha, Wajumbe wa Baraza wametembelea mradi wa SGR kipande cha kwanza ambacho ni Dar es Salaam - Morogoro ili kuona miundombinu ya ujenzi wa SGR.

Mjumbe kutoka Morogoro TRC Bi. Asha Bakari ameipongeza Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuweza kuiamini TRC na kutoa fedha kwaajili ya ujenzi wa reli ya kisasa.

"Wafanyakazi wa TRC tunatakiwa kuwa mabalozi wazuri katika kulinda huu mradi ili kuutunza kwaajili ya maendeleo ya watanzania" amesema Bi. Asha.

Bi. Oliva Benedict, mjumbe kutoka idara ya fedha makao makuu TRC amesema anaishukuru menejimenti kwa kuonesha ushirikiano kwa viongozi wa chama cha wafanyakazi na wajumbe wa idara zote za wafanyakazi katika uundaji wa baraza la wafanyakazi, pia ameipongeza TRC kwa kusimamia ujenzi wa reli ya kisasa kwani inaifanya Tanzania kuwa mfano wa kuigwa barani Afrika kupitia miundombinu ya SGR.

# KAMATI YA BUNGE YARIDHISHWA NA THAMANI YA FEDHA KATIKA MRADI WA SGR

**Na Mwandishi wetu**

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) ikiongozwa na Makamu mwenyekiti wa kamati Mhe. Japheth Hasunga imefanya ziara katika mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa – SGR kuanzia Morogoro hadi Dar es Salaam, Machi 2023.

Lengo la ziara ni kukagua mradi na kutathmini matumizi ya fedha za umma zilizowekezwa katika mradi wa SGR kwa lengo la kuleta manufaa kwa wananchi katika nyanja zote za maendeleo. Kamati ya PAC ina dhima kubwa ya kushughulikia na kusimamia matumizi ya fedha za umma katika Wizara, Idara, Wakala na Mashirika ya Umma.

"Tumetembelea ujenzi wa miundombinu ya SGR na tumepanda treni kuanzia Morogoro hadi Dar es Salaam, tumejifunza mambo mengi na tumejionea uwekezaji mkubwa umefanywa na Serikali ya awamu ya tano na ya sita" alisema Mhe. Hasunga

Makamu Mwenyekiti amesisitiza kuwa "Kamati yangu imeshuhudia mabehewa mapya ya SGR ni mazuri na mapya tofauti ya yalivyokuwa yanaonekana kwenye mitandao, kamati imeweza kuona thamani ya fedha ambazo Serikali imewekeza katika ujenzi wa miundombinu hii ya SGR"

Wajumbe wamefanya ziara kwa kutumia treni ya uhandisi ya mkandarasi wa mradi wa SGR ambapo walipata fursa ya kutembelea jengo la stesheni ya SGR mkoani Morogoro na Dar es Salaam na mabehewa ya kisasa ya SGR katika stesheni ya Pugu. Pamoja na kuona maendeleo ya mradi kipande cha Dar es Salaam – Morogoro ambacho kimefika zaidi ya asilimi 97 walipata taarifa fupi ya Shirika pamoja na mradi kwa ujumla.

Mbunge wa Viti Maalumu mkoa wa Dar es Salaam na Mjumbe wa Kamati Mhe. Janeth Masaburi amemshukuru Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kutekeleza miradi ya kimkakati kwani amefanya kazi kubwa katika miaka miwili ya uongozi wake.

"Tumetembelea yale mabehewa ambayo watu walikuwa wanayabeza, ni mabehewa mapya, mazuri yenye viwango vya kimataifa, kikubwa tunachotakiwa kufanya ni kumpa nguvu Mhe. Rais" aliongeza Mhe. Janeth

Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania Masanja Kadogosa ameishukuru kamati ya PAC kutembelea mradi wa SGR kwasababu ni miongoni mwa kamati zinazofanya kazi kwa karibu na TRC, lengo ni kuhakikisha fedha zinazotengwa zinatumiwa katika matumizi sahihi.



Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi TRC Prof. John Kondoro akiwakaribisha wajumbe wa kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) walipowasili katika stesheni ya SGR mkoani Morogoro kwaajili ya ziara kukagua mradi wa SGR kuanzia Morogoro hadi Dar es Salaam, Machi 2023.



Mkurugenzi Mkuu TRC Masanja Kadogosa akiwaelezea wajumbe wa kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) kuhusu maendeleo ya mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa - SGR, walipofanya ziara mkoani Morogoro hadi Dar es Salaam, Machi 2023.

# KAMPENI YA UELEWA KUHUSU MRADI WA SGR KIPANDE CHA NNE TABORA –ISAKA YAANZA



**Na Mwandishi wetu**

Shirika la Reli Tanzania limeanza utoaji wa elimu kwa wananchi wa mkoa wa Tabora kuhusu mradi wa SGR kipande cha nne Tabora – Isaka chenye jumla ya kilomita 165, Machi 2023.

Meneja msaidizi wa mradi wa SGR kipande cha nne Mhandisi Abduli Habib akiwa na watendaji wa kada mbalimbali kutoka TRC walifika ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Tabora na kuonana na Kaimu Afisa Tawala wa Mkoa wa Tabora Ndugu Daniel Barangu na kumueleza lengo la kampeni ya uelewa wa mradi wa SGR kipande cha nne, ni kuwaelimisha wananchi kuhusu mradi wa SGR na mambo mengine yatakayowagusa wananchi watakaopitiwa na mradi ikiwemo kutwaliwa ardhi yao. Wananchi watajulishwa utaratibu utakaotumika kupima ardhi na ulipaji fidia kwa vyote ambavyo haviamishiki vitakavyokutwa kwenye ardhi .

Mhandisi Abdul Habib amemjulisha Kaimu Afisa Tawala Mkoa wa Tabora kuwa wananchi watapewa elimu kuhusu ulinzi na usalama wa reli, watajulishwa mambo ya kuzingatia ili kudumisha uhusiano mwema kati ya jamii na watekelezaji wa mradi, watapatiwa elimu kuhusu mazingira, utaratibu wa kupata ajira kwa mkandarasi, wataelekezwa utaratibu wa kuwasilisha maoni au malalamiko kuhusu mradi na mwisho watapewa nafasi ya kuuliza maswali na kupatiwa majibu.

Ndugu Baragu ameipongeza TRC kwa utoaji elimu mapema kuhusu mradi wa SGR na kusema kuwa wananchi wanayo maswali ambayo yanahitaji ufafanuzi, elimu kutolewa kabla ya mradi kuanza itapunguza malalamiko kwa kuwa wananchi watakuwa na uelewa kuhusu mradi na stahiki watakazolipwa kwa maeneo yatakayopitiwa na mradi.

"Mradi wa SGR kwa mkoa wa Tabora utakuwa na manufaa makubwa kwa wananchi, natoa wito wakazi wote wanaopitiwa na mradi kutoa ushirikiano kwa TRC na Mkandarasi ili kuhakikisha mradi huu haukwami" alisema Ndugu Barangu

Mkuu wa Wilaya ya Tabora Mhe. Luis Peter Bura amesema wanatarajia ajira zitakazotolewa na mkandarasi zitatoa kipaumbele kwa wananchi wenye sifa wanaopitiwa na mradi.

"Ni aibu kwa wakazi wa Tabora wanaopewa ajira na Mkandarasi na kugeuka wezi wa mali za Mkandarasi, sifa mama ya kuajiriwa iwe ni uaminifu" alisisitiza Mhe. Bura.

Kampeni ya uelewa kuhusu mradi wa SGR kipande cha nne Tabora – Isaka itafanyika kwa zaidi ya wiki mbili katika Wilaya ya Tabora, Uyui na Nzega katika vijiji thelathini na moja (31).

# MAAFISA UHUSIANO NA MAWASILIANO YA SERIKALI WATEMBELEA MRADI A SGR

**Na Mwandishi wetu**

Maafisa Uhusiano na Mawasiliano Serikalini wakiongozwa na Msemaji Mkuu wa Serikali Bwana Gerson Msigwa watembelea mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa – SGR kuanzia Dar es Salaam hadi Soga mkoani Pwani, Machi 2023.

"Ni vizuri wanahabari wenye jukumu la kuwaambia watanzania wakatoa taarifa sahihi kupitia kuona. Wamefurahi kutembelea mradi kutoka Dar es Salaam hadi Soga mradi unakwenda vizuri. Mkakati wetu ni kuhakikisha maafisa habari wanapata taarifa za kutosha ili wawe katika nafasi nzuri ya kuwaambia watanzania faida za miradi inayotekelezwa na Serikali ya Dkt. Samia Suluhu Hassan" alisema Msigwa.

Msigwa aliongeza kuwa lengo lilikuwa ni kuhakikisha maafisa habari wanapata uelewa kuhusu kazi zinazofanywa na Serikali, maafisa habari ndio wanaofanya kazi ya kusema kwa wananchi. Maafisa habari wote wamepata nafasi ya kuja kuona kazi kubwa inayofanywa na Serikali kwasababu nchi yetu inapita katika kipindi ambacho inaandika historia kubwa.

"Tumejitahidi kuhakikisha tunawapa nafasi na tumewapitisha katika vituo vyote ambako mradi huu unatekelezwa, kituo chetu cha kwanza Dar es Salaam, wameona kituo cha kisasa na mifumo yake ya kuendeshea treni, pia tumewapeleka Pugu wameona kituo na mabehewa, tumewapeleka Soga na wameona kazi kubwa iliyofanyika" alisema Msigwa

Ziara imefuatia baada ya kikao kazi cha 18 cha Maafisa Habari na Mawasiliano Serikalini kilichofanyika katika ukumbu wa mikutano wa Mwl. Nyerere jijini Dar es Salaam kuanzia Machi 27 hadi 31 2023 kwa lengo la kubadilishana uzoefu na kuwajengea uwezo maafisa habari katika majukumu yao.



Mkurugenzi Mkuu wa TRC Ndugu Masanja Kungu Kadogosa akitoa maelezo ya namna ya ukataji wa tiketi za treni za kisasa kwa Maafisa Habari, Uhusiano na Mawasiliano wa Serikali walipotembelea kuona maendeleo ya ujenzi wa mradi wa reli ya kisasa - SGR katika jengo la stesheni ya SGR lililopo jijini Dar es Salaam, Machi 2023.



Kaimu Mkurugenzi wa Ujenzi na Miundombinu ya Reli TRC Mhandisi Machibya Masanja (aliyeshika kipaza sauti) akiwaelezea Maafisa Habari, Uhusiano na Mawasiliano wa Serikali kuhusu ubora na uimara wa tuta la SGR walipotembelea kuona maendeleo ya ujenzi wa mradi wa reli ya kisasa - SGR katika jengo la stesheni ya SGR lililopo jijini Dar es Salaam, Machi 2023.



Meneja Mradi wa SGR kipande cha Dar es Salaam - Morogoro Mhandisi Thadey Komu akiwaelezea Maafisa Uhusiano na Mawasiliano Serikali kuhusu maendeleo ya mradi walipofanya ziara katika Stesheni ya Soga hivi karibuni Machi 2023.




BODI YA WAHARIRI
MHARIRI MKUU | Jamila Mbarouk, MHARIRI MSAIDIZI/MSANIFU | Sami Omary
HABARI | Hemed Mohamed, Mariam Katunge MAKALA | Aziza Charles, Amina Juma, Athumani Iddy
PICHA | Musa Kadiko, Hassan Mbonde, Augustino Bulegea